

# Nyenzo ya Shirika Kujiangaliza (OMT)



FORDFOUNDATION

## (OMT) NYENZO YA SHIRIKA KUJIANGALIZA KWA KINA- FOMU BINAFSI

Nyenzo ya Shirika Kujiangaliza (OMT) iliandaliwa ili kuwasaidia wafanyakazi wa shirika husika kutafakari uwezo washirika hilo na kubainisha maeneo ya kuiimarisha taasisi husika iliiweze kujengamwafaka shirikani.Uchunguzi huu unatoa fursa kwa shirika lenu kujitafakari lenyewe kwa ujumla, kwa kujiuliza kitu gani kinafanyika vizuri na kitu gani kingeweza kuboreshwa, na hivyo kuwasaidia kwa pamojakubainisha maeneo ya kupewa kipaumbel ili kuboresha napia hatua za kuchukua kufanya hivyo

Nyenzo ya Shirika Kujiangaliza (OMT) imeandaliwa kuyafaa mashirika yenyeye ukubwa au udogowowote i na hata viwango tofauti nya kiuwezo –kuanzia mashirika madogo au mashirika mapya hadi mashirika yaliyokomaa na mashirika yenyeye masuala tata ..

Nyenzo hii inapaswa kujazwana wafanyakazi wote –wa programu mbalimbali na wa utawala–na,kadri inavyofaa, wajumbe husika wa chombo kikuu cha utawala (ambacho wakati mwingine hujulikana kama bodi ya wakurugenzi), maana mitazamo mbalimbali ina thamani katika kufahamu fika uwezo wa shirika lenu na maeneo yanayohitaji kukuzwa..

Mchakatohuu utafaa zaidi iwapo utafanya na mtu ambaye si mfanyakazi au mjumbe wa bodi akiwa ndio mwezeshaji. Zoezi hili linaweza kufanyika kwa njia mbili: ama washiriki kujaza fomu hii mmoja mmoja kabla ya zoezi kuanzai , au kujaza fomu hii wakatizoezi lenyewe linapoanza.. Mwezeshaji wenu atawaeleza iwapo mtapaswa kujaza fomu hii kabla ya zoezi au la.Iwapo mtajaza fomu hii kabla yazoezi, tafadhali komea mwishoni mwa ukurasa wa 24. Mtapaswa tu kujaza fomu hii kuanzia ukurasa wa 25 na kuendelea mtakapotakiwa namuwezeshaji kufanya hivyo.

Mambo machache ya kuzin gatia:

- Vipengele mbalimbali katika fomu hii vinakusudia kuwasaidia kulitafakari shirika lenu kwa kufuata mpangilio wa majibu ifuatavyo: Kiwango cha Chini, Kiwango cha Kawaida, Kiwango cha Wastani, na Kiwango Kikuu.
- Tafadhali usitiliemaanani sanakkiwango cha maalum chaushindi au “matokeo”, cha muhimu ni kuelewa wapi unafikiri shirika lenu lipo.Thamani kuu ya nyenzo hii ipo kwenye majadiliano ya pamoja.
- Iwapo utashindwa kufanya uchaguzi kati ya majibu mawili (kwa mfano, kati ya Kiwango cha Kwaida na Kiwango cha Wastani), unaweza kuweka alama ya mduara katikati ya majibu hayo mawili kuonesha kwamba unamaanisha jibu sahihi lipo mahali fulani katikati ya majibu hayo mawili.
- Kumbuka kuwa hakuna shirika linalotarajiwa kuwa na “ uwezo” kwenye vipengele vyote.
- Tafadhali tumia sehemu ya Maoni, ambayo inapatikana mwishoni mwa kila sehemu, kufanua uchaguzi wako, hasa iwapokama utakuta maelezo ya sasa hayashabihiani kabisa na shirika lenu.Haya yanaweza kuwa maelezo ambayo si rasmi ambayo unaweza kuyarudia baadaye wakati wa majadiliano ya pamoja.Maoni hayo ni kwa ajili ya rejea yako tu hayataangaliwa wala kukusanya na mwezeshaji.
- Tafadhali usiwaulize wengine jinsi wanavyojibu kabla ya wewe mwenyewe kujaza fomu hii. Haya yanapaswa kuwa majibu yako – kutakuwepo na muda mzuri baadayekufikia mwafaka wapamoja..
- Iwapo unafikiri kuna swali halibusiani kabisa na shirika lenu, achana nalo usilijibu. Lakini iwapo unafikiri endapo swali hilo lingelizwa kwanjia nyingine lingeweza kuhusiana na shirika lenu, hifadhi maoni yako kwenye Sehemu ya Maoni ya jinsi ambavyo ungetaka swalihilo liulizwe.

Mwezeshaji wenu atakisaidia kikundi kufikia mwafaka wa jibu la kiwango kwa kila kipengele. Tena, tafadhali subiri kabla ya kukamilisha zoezi la kuamua maeneo ya kupewa kipaumbele mwishoni mwa ujazaji fomu hii hadi mwezeshaji atakapowataka kufanya hivyo,wakati mtakapokua mmefikia mwafaka kwa pamoja.Baada ya hapo utatakiwa tena kuchagua kipaumbele cha kwanza, cha pili na cha tatu katika uimarishaji wa shirika lenu.

Kitakachokua tofauti ni katika Uongozi wa juu Kiutendaji.Sehemu hii, na swali la mwisho, vinakusudiwa kujibiwa na kila mshiriki bila kuonesha jina lake kisha kuwasilishwa kwa mwezeshaji, ambaye atabainisha jibu linaloonyesha kiwango muafakakutokana na majibu yote yaliyoandikwa.

Baadaye muwezeshaji atawaongoza kama kikundi kuititia zoezi la kubainisha vipaumbele vya pamoja vya shirika lenu kwa ajili ya uimarishwaji wa kitaasisi Jambo hili litafutiwa na majadiliano kuhusu njia bora zaidi za kufanikisha mabadiliko ambayo mmeyapatia kipaumbelena yatakayosaidiakufanua matokeo mnayoyatarajia,, mikakati, muda nawatu wanaohusika kwenye kazi ya uimarishaji wa taasisi yenu.

Kwa kuwa huu ni mchakato wenu, mnawenza kuamua jinsi ambavyo mtashirikishamatokeo yake kwa hadhiranje ya shirika..Baada yazoezi hili la kujiangalizakukamilika, muwezeshaji atawashirikisha viongozi wenu wa shirika matokeo yake, ambao ndio watapitia upya ripoti na kuamua mambo yapi yatashirikisha nje ya shirika, iwapo yapo. Asante kwa kutenga muda kuchangia mtazamo wako!

## Dhima na Mkakati

|                           | Kiwango cha Chini  | Kiwango cha Kawaida  | Kiwango cha Wastani  | Kiwango Kikubwa   |
|---------------------------|--|--|--|---|
| <b>Dhima na Dira</b>      | Hakuna dhima wala dirailiyo kimaandishi na hakuna maadili yanayotawala utendaji kazi ambayo kila mmoja ameshirikishwa. | Dhima na Dira vimeandikwa lakini ni tata; wengi shirikani hawawezi kuvielezea kwa ufasaha.   | Ufafanuzi wa dhima na dira ya shirika ni wazi; ila ungeweza kuwa bayana zaidi, wafanyakazi wengi wanauelewa na wanaonyesha moyo wakuendana navyo.                      | U dhima ya shirikaiko wazi, mahususi, nayakuvutia sana na dira ni yenye kuhamasisha; wafanyakazi na bodi wote wanaiamini na kuiishi na dhima na dira hiyo.  |
| <b>Malengo na Matokeo</b> | Hakuna malengo na matokeo kwa ajili ya kazi za programu za kazi mbalimbali za shirika ambayo yameelezwa kwa ufasaha.   | Lengo la muda mrefu limeelezwa, lakini sio thabit au halitekelezeki na hakuna matokeo ya muda mfupi.Ni wafanyakazi na wajumbe wa bodi wachache tu wanaoweza kuyaelezea haya. | Lengo na matokeo yakoi wazi, lakinihatathminiki kirahisi.Japo yanafahamika na walio wengi shirikani, hayatumiki kutoa mwongozo kwenye program na kazi za kiuendeshaji. | Lengo ni wazi na matokeo yanatekelezeka na yanatathminika na yanafahamika shirikani; yanatoa mwongozo kwa kazi za programu na za kiuendeshaji.  |
| <b>Mpango Mkakati</b>     | Hakuna mpango mkakati ulioandikwa na kazi za shirika hazina mwelekeo walamuingiliano kati ya mirad.                    | Mpango mkakati umeandikwa lakini hautoi mwongozo wazi kwa kazi ya shirika; unarejelewa kwa nadra sana.   | Mpango mkakati unatoa mwongozo wa jumla kwa ajili ya kazi za programu mbalimbali na za uendeshaji lakini hautoi mwongozo mara kwa mara wa kufanya maamuzi.             | Mpango mkakati una mwelekeo wazi kuhusu matokeo na athari na huongoza kufanya maamuzi. Programu mbalimbali zinapitipa upya mara kwa mara na kurekebishwa kulingana na changamoto na fursa mpya ili kuhakikisha zinafungamanishwa kwenye mpango mkakati. |

**Maoni:**

## ■ Maandalizi ya Programu Mbalimbali

|   | Kiwango cha Chini  | Kiwango cha Kawaida  | Kiwango cha Wastani   | Kiwango Kikubwa  |
|---|--|--|---|--|
| <b>Kufungamana kwa Dhima na Programu Mbalimbali</b>               | Miradi mbalimbali haifungamani moja kwa moja na dhima au malengo; kazi kubwa hufafanuliwa na miradi tofauti na huru ambayo haikuunganishwa pamoja.     | Miradi mingi inaweza kufungamana na dhima na malengo lakini ni vigumu kwa shirika kufafanua wazi kitu kipi kinaingia kwenye dhima yake au hakitakiwi kuingia; kila mradi unatekelezwa peke yake pasipo kuhusishwa na miradi mingine. | Miradi tofauti inafungamanishwa kwenye programu mbalimbali ambazo zimefanuliwa vizuri na zinapatana na dhima na malengo ya shirika. Programu kwa kawaida huendeshwa pasipo kuhusishwa na programu nyingine. | Programu zote zimefanuliwa vizuri na zimefungamanishwa kikamilifu na dhima na malengo; programu mbalimbali zimeunganishwa pamoja na huendeshwa kwa kushauriana baina yao ili kuhakikisha kunakuwepo na ufanisi wa hali ya juu. |
| <b>Upangaji Programu</b>  | Upangaji programu hutokea kwa nadra na huwa hauhusishi tathmini za fursa au mahitaji.  | Upangaji progamu hutokea lakini huwa hauhusishi tathmini rasmi za fursa au wauchambuzi mahitaji.   | Uchambuzi wa za fursa au mahitaji hufanyika na kuhifadhiwa kimaandishi na mikakati ya programuhurejewa upya mara moja moja kulingana na tathmini zisizo rasmi.  | Programu mbalimbali hutayarishwa kutokana na uchambuzi wafursa au mahitaji ambazo zilihifadhiwa kimaandishi; zinatathmniwa na kurejewa upya mara kwa mara kuhakikisha kwamba zinabaki kuwa na ufanisi wa hali ya juu sana.     |
| <b>Ujumuishaji wa Sauti ambazo Kihistoria Zimeachwa pembezoni</b> | Sauti za vikundi kwenye jamii ambavyo kihistoria huwa vimeachwa pembezoniambavyo shirika linafanya kazi navyo hazifikiriwi katika maamuzi ya programu. | Sauti za vikundi ambavyo kihistoria huwa vimeachwa pembezoniuhufikiriwa mara moja moja katika maamuzi ya programu.   | Sauti za vikundi ambavyo kihistoria vimeachwa pembezoni mara moja moja katika maamuzi ya programu.  | Sauti za vikundi ambavyo kihistoria vimeachwa pembezoni kwenye jamii ambazo shirika linafanya nazo kazi zinasakwa kivitendo na zina ushawishi dhahiri katika utayarishaji programu mbalimbali.                                 |

**Tafadhali ainisha vikundi unavyofikiri kuwa kihistoria huwa vinawekwa pembezoni.**

Mifano inaweza kujumuisha: "wanawake wa vijijini," "watu wenye ulemavu," "jamii za asili."

**Maoni**

## Kujifunza na Tathmini

|  | Kiwango cha Chini  | Kiwango cha Kawaida  | Kiwango cha Wastani   | Kiwango Kikubwa  |
|--|--|--|---|--|
| <b>Tathmini ya Programu</b>            | Tathmini ya programu hazifanyika   | Tathmini za programuhufanyika kiholela na hazihusishwi na vipaumbele nya shirika, nadharia ya mabadiliko au madhumuni ya kujifunza; taarifa hii haitoi mwongozo wowote kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kimkakati au kujifunza shirikani. | Tathmini za programzinafanyika lakini hazihusishwi vizuri na vipaumbele nya shirika, nadharia ya mabadiliko au madhumuni ya kujifunza; taarifa hii inaweza kutumika au kutotumika kutoa mwongozo kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kimkakati aukujifunza shirikani.     | Tathmini za programuzenyi kufuata utaratibu maalumu hufanyika na kwa kawaida zinafanuliwa na vipaumbele nya shirika, nadharia ya mabadiliko na/au madhumuni ya kujifunza; mafunzo yanayopatikana hutoa taarifa mwafaka ambazo huwezesha kufanyika maamuzi ya kimkakati na kijifunza shirikani. |
| <b>Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data</b> | Hakuna mfumo rasmi wa ukusanyaji nauchambuziwa data.   | Kuna mfumo wa msingi wa ukusanyaji na uchambuzi wa data lakini hautumiki mara kwa mara; unaweza hata kuonekana kama udhia usiokuwa na msaada wowote kwene ufuutiliaji wa maendeleo kuelekea matokeo.                                     | Mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi wa data inatumika lakini ingeweza kutayarishwa vizuri zaidi ili iweze kuhusiana na kuwasaidia zaidi wale wanaoitumia. Ushahidi ambaa umekusanywa hutoa baadhi ya taarifa muhimu kwa ajili ya kufuatilia maendeleo kuelekea matokeo. | Mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi wa data imechangamana ipasavyo na kazi za shirika na kuonekana kuhusiana na kuwasaidia wale wanaoitumia. Ushahidi ambaa umekusanywa hutoa taarifa muhimu kwa ajili ya kufuatilia maendeleo kuelekea matokeo.   |
| <b>Athari ya Tathmini kwa Shirika</b>  | Hakuna shauku ya kutafakari na kujifunza na hakuna matarajio kwamba ushahidi unaopatikana utasababisha uboreshaji wa mkakati na utendaji kazi. | Kuna shauku kidogo na rasilimali haba kwa ajili ya kutafakari na kujifunza; kuna ushahidi mchache sana unatumika kuboresha mkakati na utendaji kazi.   | Japo kuna shauku ya kutafakari na kujifunza, kuna rasilimali ndogo kuhakikisha kutafakari na kujifunza vinafanyika mara kwa mara; maboresho ya mkakati na utendaji kazi yanafanyika kulingana na ushahidi uliopatikana, lakini kiholela.                              | Kuna utamaduni wa kutafakari na kujifunza na rasilimali zipo na zinatumika kuhakikisha kujifunza kutohana na ushahidi na uzoefu uliopatikana kunatokea. Funzo liliopatikana husababisha maboresho ya mkakati na utendaji kazi na mafunzo haya yanashirikishwa ndani na nje ya shirika.         |

**Maoni:**

## Utetezi

|   | Kiwango cha Chini   | Kiwango cha Kawaida   | Kiwango cha Wastani  | Kiwango Kikubwa  |
|---|---|---|--|--|
| <b>Mkakati wa Utetezi</b>                     | Kuwashawishi waundaji wa sera au kuwajibisha vikundi lengwa si sehemu ya kazi za shirika.                 | Kuwashawishi watungaseru au kuwajibisha vikundi lengwakunahusiana na kazi za shirika lakini hakufanyiki kwa utaratibu maalumu ila kiholela.   | Kuwashawishi watunga sera au kuwajibisha vikundi lengwani sehemu ya mkakati wa msingi wa shirika, lakini sikuzote kufanya hivyo hakutokani na mwongozo wa mkakati wa uteteziambao ni wazi na wa kueleweka.     | Mkakati changamano wa utetezi unatumika na unaathiri utengaji sera au unawajibisha vikundi lengwa kiutendaji na kimwitikio.  |
| <b>Kujihusishana Masuala ya Kisasa</b>        | Maendeleo ya kisasa hayafuatiliwi kwa karibu.   | Maendeleo ya kisasa yanafuatiiliwa kiholela bila mpangilio maalum   | Maendeleo ya kisasa yanafuatiiliwa kwa utaratibu maalumu, lakini kuna ubaha wa taarifa "za ndani."   | Maendeleo ya kisasa yanafuatiiliwa kwa karibu, na wafanyakazi wana taarifa "za ndani" ambazo zinawawezesha kuitikia haraka nakwa kimkakati kwa maendeleo mapya ya kisasa.  |
| <b>Ukaribu wa shirika kwa wenyewe mamlaka</b> | Hakuna utayari wala ujuzi au wahusika wa kushiriki katika majadiliano huru ya kujadili sera/ uwajibikaji. | Kuna utayari na ujuzi kidogo wa kushiriki katika majadiliano ya kujadili sera/uwajibikaji lakini shirika halina wahusika wanaowezaa kushawishi majadiliano hayo (au kinyume chake). | Kuna utayari na ujuzi na baadhi ya mawasiliano kiasi ya kushawishi majadiliano ya kujadili sera/ uwajibikaji lakiniviti hivyo vinahitaji kuimarishe.   | Wafanyakazi wanaheshimiwa sana na mara kwa mara wanaitwa kushiriki au kuongoza majadiliano ya kujadili sera/uwajibikaji katika ngazi za kijamii, kitaifa, au kimataifa.  |
| <b>Mapendezo ya Kisera</b>                    | Hakuna mapendekezo ya kisera wazi au ya uhakika na kweli.   | Kuna baadhi ya mapendekezo ya kisera lakini yangeweza kuwa wazi zaidi, ya uhakika na kweli zaidi, na kurekebishwa zaidi kulingana na hadhira inayolengwa.                           | Mapendekezo ya kisera wazi na ya uhakika na kweli yanatolewa kwa hadhira mwafaka inayolengwa, lakini yangeweza kupitwa upya mara kwa mara ili yaweze kuzingatia mabadiliko mbalimbali ya kisasia yanayojiteza. | Mapendekezo ya kisera yako wazi na ya uhakika na kweli yanatolewa na kurekebishwa kulingana na dhima na mpango mkakati wa shirika, kadri inavyotakiwa, na utashi wa kisasia na mabadiliko mbalimbali yanayojiteza. |

## ■ Utetezi, unaendelea

|                | Kiwango cha Chini   | Kiwango cha Kawaida   | Kiwango cha Wastani   | Kiwango Kikubwa   |
|----------------|---|---|---|---|
| <b>Utafiti</b> | Kuna uahamu mdogo kuhusu utafiti unaoendelea na uhusiano wake na utetezi. | Kuna uahamu kidogo kuhusu utafiti unaoendelea kuhusiana na utetezi, lakini haukuunganishwa ipasavyo kwenye kazi ya utetezi. Shirika limefanya utafiti kidogo tu au halijafanya kabisa utafiti wowote lenyewe. | Utafiti wa nje mara nyingi unatumia kwenye utetezi; pale inapobidi, shirika hufanya utafiti unaoziba mapengo kwenye shughuli zake za ugani. | Utafiti wa nje katika utetezi unatumika ipasavyo na, pale inapobidi, shirika hufanya utafiti wake lenyewe ambaa unachangia kwenye shughuli zake za ugani, na kuunganishwa katika kazi za kisera zinazodhihirisha utendaji bora. |

Maoni:

## Kujishughulisha na Kazi za Uwandani

|   | <b>Kiwango cha Chini</b>   | <b>Kiwango cha Kawaida</b>   | <b>Kiwango cha Wastani</b>  | <b>Kiwango Kikubwa</b>  |
|---|--|--|---|---|
| <b>Ushirikiano Bainaya Shirika na Wadau Wengine</b>   | Kuna ufahamu kidogo kuhusu kuwepo na kutokuwepo ushirikiano wowote baina ya shirika na wadau wengine wakuu kwenye shughuli za ugani. | Kuna ufahamu kuhusu wadau wakuu kwenye shughuli za ugani lakini kuna ushirikiano mdogo wa moja kwa moja baina ya shirika na wadau hao. | Kuna ufahamu wa wadau wakuu kwenye shughuli za ugani na ushirikiano kiasi wenye tija na wadau hao.                        | Kuna ushirikiano mkubwa wenyetija na wadau wakuu kwenye shughuli za ugani kwenye ngazi za kijamii, kitaifa, kimko na/ au kimataifa                    |
| <b>Ushiriki wa Shirika kwenye Mitandao Mbalimbali</b> | Hakuna ushiriki kivitendo kwenye mitandao mbalimbali   | Shirika ni mshiriki wa mara moja moja kwenye mitandao mbalimbali na mishikamano mingine mbalimbali.                                    | Shirika mara nyingi ni mshiriki hai kwenye mitandao mbalimbali na mishikamano mingine lakini si kwenye nafasi ya uongozi. | Shirika ni kiongozi hai kwenye mitandao mbalimbali na mishikamano mingine ambayo inafafanua na kusukuma ajenda mbalimbali.                            |
| <b>Jukumu la Shirika kwenye harakatiza mabadiliko</b> | Shirika halijioni kuwa sehemu yaharakatiza mabadiliko na hutenda kazi lenyewe.   | Shirika hujiona kuwa sehemu ya harakati za mabadiliko lakini halitoi mchango wowote dhahir   | Shirika ni hai kwenye harakati za mabadiliko lakini pasipo kuwa na mbinu mkakati kamilifu                                 | Shirika linabainisha jukumu lake la kimkakati kwenye harakati za mabadilikona linatoa michango dhahiri na kwa utaratibu maalumu kwenye vuguvugu hilo. |
| <b>Hadhi ya Shirika katika Ugani</b>                  | Shirika lina hadhi ya kutoshirikiana na wadau wengine katikaugani.   | Shirika lina hadhi ya kufanya vizuri na idadi ndogo ya mashirika lakini sio na baadhi ya mashirika mengine.                            | Shirika linafanya vizuri na mashirika mengine na mashirika yaliyo mengi yanasisia hadhi yake.                             | Shirika linafikiriwa kuwa mfano wa kuigwa hasa kuhusiana na ushirikiano na kufanya kazi kama timu moja na hadhi yake inadhihirisha jambo hili.        |

**Maoni:**

## ■ Uongozi wa Kimtandao

Zingatia: Sehemu hii inapaswa kujazwa tu na mitandao na mishikamano.

|                             | Kiwango cha Chini   | Kiwango cha Kawaida   | Kiwango cha Wastani  | Kiwango Kikubwa   |
|-----------------------------|---|---|--|---|
| <b>Mkakati wa Mtandao</b>   | Mtandao hauna mkakati ulioelezwa kwa ufasaha au mwelekeo amba ni tofauti na mashirika walio wanachama wake.                                     | Mtandao una mkakati ulioelezwa kwa ufasaha kiasi lakini kwa sehemu kubwa unategemea sana mikakati ya wanachama wake, kiasi kwamba wakati mwininge inakuwa vigumu kuutofautisha mtandao na wanachama wake.                   | Mtandao una mkakati ulioelezwa kwa ufasaha amba mara moja moja huingia doa kutokana na mikakati ya wanachama wake.                                     | Mtandao una mkakati wa kuvutia sana na ulioelezwa kwa ufasaha amba ni tofauti lakini hukamilishwa na mikakati ya wanachama wake.                                |
| <b>Msimamo Thabiti</b>      | Mtandao hauna ulinganifu kati ya mawasiliano yake na utetezi wake, jambo ambalo huusababisha mtandao kutokuwa hai kiutendaji.                   | Mtandao ni hai kiutendaji unapokuwa unaitikia matukio muhimu lakini vinginevyo mara nydingi huwa ni mtandao uliobweteka tu..  | Kwa kawaida mtandao ni hai kiutendaji kwenye mambo yake, lakini ungeweza kuwa na ufanisi zaidi katika mawasiliano yake na wanachama na hadhira ya nje. | Mtandao una ufanisi mkubwa, na unajihuisha na wanachama na hadhira ya nje kwa utaratibu maalumu kiutendaji.   |
| <b>Utatuuzi wa Migogoro</b> | Migogoro au kutoelewana mionganoni mwa wanachama huzuia kushirikiana au kushirikishana rasilimali; mtandao huwa hausuluhihi mivutano kama hiyo. | Migogoro au kutoelewana hujitokeza mara kwa mara mionganoni mwa wanachama na mara nydingi huzuia ushirikiano unaofaa au kushirikishana rasilimali; juhud za mtandao za kusuluhihi mivutano mara nydingi huwa hazifanikiwi.. | Kutolelewana mionganoni mwa wanachama hujitokeza mara moja moja lakini hutatuliwa kwa kutumia njia nzuri.  | Migogoro mionganoni mwa wanachama ni nadra sana na, inapojitokeza, hutatuliwa vizuri na mtandao kwa jinsi ambayo huruhusu kuendelea kuwepo ushirikiano unaofaa. |

**Maoni:**

## Mawasiliano ya Nje

|   | <b>Kiwango cha Chini</b>   | <b>Kiwango cha Kawaida</b>   | <b>Kiwango cha Wastani</b>   | <b>Kiwango Kikubwa</b>   |
|---|--|--|--|--|
| <b>Mkakati wa Mawasiliano</b>                                       | Shirika linajishughulisha kwa nadra sana na shughuli za nje ya shirika na hakuna mkakati wa kufanya hivyo; walengwa wakuu hawajabainishwa. | Hakuna mkakati rasmii wa mawasiliano shirikani lakini shirika mara moja moja hujishughulisha na shughuli za nje ya shirika za kawaida fursa zikijitokeza     | Kuna mkakati wa mawasiliano shirikani lakini haupatani na hadhira lengwa na jumbe huwa hazirekebishwi kulingana na miktadha inayobadilkabadiika.                         | Kuna mkakati wa mawasiliano ulioelezewa vizuri ukiwa na jumbe tofauti zikilenga hadhira lengwa ambazo zinarekebishwa mara kwa mara kwa kuzingatia miktadha inayobadilkabadiika.        |
| <b>Ulinganifu wa Lengo na Ujumbe</b>                                | Jumbe kuu wakati mwininge haziungi mkono malengo ya shirika na hata huyadhoofisha.   | Jumbe kuu kwa kawaida huunga mkono malengo ya shirika lakini hazipatani na malengo hayo.   | Jumbe kuu kwa kutumia utaratibu maalumu huunga mkono malengo ya shirika.   | Jumbe kuu kwa kutumia utaratibu maalumu zinafa sana uendelezaji wa malengo ya shirika.   |
| <b>Mwitikio wa Shirika Dhidi ya Mashambulizi Dhidi ya Kazi Yake</b> | Mashambulizi dhidi ya shirika yanapotokea, hayagunduliki, na shirika haliyaitikii.   | Shirika hugundua baadhi ya mashambulizi yanayojoitekeza dhidi yake na huitikia baadhi ya mashambulizi na hupata mafanikio kiasi.                             | Shirika hugundua mashambulizi mengi yanayojoitekeza dhidi yake na huitikia mashambulizi mengi kwa wakati na kwa kutumia njia inayofaa.                                   | Mashambulizi dhidi ya shirika yanapojitekeza, yanagundulika na kushughulikiwa kwa wakati na kwa kutumia njia inayofaa.   |
| <b>Usambazaji wa Taarifa za Shirika</b>                             | Shirika halisambazi taarifa kwa hadhira muhimu.  | Shirika linasambaza taarifa, lakini halirekebishi jumbe kwa ajili ya hadhira lengwa tofauti  | Kwa ujumla shirika husambaza taarifa kwa hadhira lengwa, lakini lingeweza kuhakikisha zinakwenda zaidi na wakati, zinahusiana na hadhira lengwa, na kuwa mahususi zaidi. | Kwa ujumla shirika husambaza taarifa zake kwa wakati na kwa kutumia maumbo yanayofikika kirahisi na hadhira lengwa, na huwasilisha jumbe zinazoeleweka na mahususi kwa hadhira muhimu. |
| <b>Zana za Mawasiliano</b>  | Shirika halina zana za kutumia kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa.  | Shirika linatumia zana za msingi tu lakini ambazo zimepitwa na wakati kwa ajili ya kazi za nje ya shirika lakini si kila mara zinafa kufikia hadhira lengwa. | Zana kwa sehemu kubwa ni mwafaka kwa hdhira lengwa, lakini hazitumiki kikamilifu.  | Zana zimeandalowi vizuri sana, zinifikika kirahisi, na zinatumika kikamilifu kuifikia hadhira lengwa.  |

**Maoni:**

## ■ Utawala

**Zingatia:** “Chombo kikuu cha utawala” kinamaanisha kikundi ambacho kiutendaji huhusika kwenye kulitawala shirika (kwa kawaida ni Bodi ya Wakurugenzi).

|   | Kiwango cha Chini   | Kiwango cha Kawaida  | Kiwango cha Wastani  | Kiwango Kikubwa  |
|---|---|--|--|--|
| <b>Muundo wa Chombo Kikuu cha Utawala</b>                       | Wajumbe wa chombo kikuu cha utawala wanatokana na nyanja chache, wana uzoefu mdogo stahiki, na hawajumuishi makundi ambayo kihistoria huwa yanaenguliwa.  | Wajumbe wa chombo kikuu cha utawala wanatokana na nyanja chache; kuna uwakilishi mdogo wa makundi ambayo kihistoria huwa yanaenguliwa; baadhi ya wajumbe wana uzoefu stahiki.                                  | Wajumbe wa chombo kikuu cha utawala wanatokana na baadhi ya nyanja stahiki na wanajumuisha makundi ambayo kihistoria huwa yanaenguliwa; wajumbe wengi wana uzoefu stahiki kiasi.               | Wajumbe wa chombo kikuu cha utawala wanatokana na nyanja mbalimbali nydingi stahiki; makundi ambayo kihistoria huwa yanaenguliwa yanawakilishwa vizuri; wajumbe wana uzoefu mwiningi na utaalamu wa kivitendo.                                       |
| <b>Sera za Chombo Kikuu cha Utawala</b>                         | Hakuna sera za chombo kikuu cha utawala kuhusu, kwa mfano, masuala kama vile kikomo cha kuwa mjambe, mgongano wa kimaslahi, au maelekezo ya mazingira ya shirika kwa chombo hicho.                        | Sera za chombo kikuu cha utawala zipo lakini hazizingatiwi kwa masuala kama vile, kikomo cha kuwa mjambe, na maelekezo ya mazingira ya shirika kwa chombo hicho.   | Sera za chombo kikuu cha utawala zipo na zinazingatiwa kwa masuala kama vile, kwa mfano, kikomo cha kuwa mjambe, mgongano wa kimaslahi, na maelekezo ya mazingira ya shirika kwa chombo hicho. | Sera za chombo kikuu cha utawala kwa masuala kama vile, kwa mfano, kikomo cha kuwa mjambe, mgongano wa kimaslahi, na maelekezo ya mazingira ya shirika kwa chombo hicho zinadhahirisha utendaji mzuri na zinafautiliwa kwa karibu.                   |
| <b>Mikutano ya Chombo Kikuu cha Utawala</b>                     | Mikutano inafanyika mara moja moja, wajumbe wachache tu huhudhuria, kumbukumbu zake hazihadhiwi vizuri kimaandishi, na/au husababisha maamuzi ambayo si wazi kufanyika; mara nydingi mivutano hujitokeza. | Mikutano hufanyika mara kwa mara lakini sikuzote hahihadhiwi vizuri au kumbukumbu zake hazihadhiwi kimaandishi; mara nydingi husababisha maamuzi ambayo si wazi kufanyika; mivutano hujitokeza mara moja moja. | Mikutano mingi hufanyika vizuri, inahudhuriwa vizuri na kumbukumbu zake hahihadhiwi vizuri; maamuzi hufanyika kwa uwazi. Mikutano huwa haitoi fursa ya kutosha kwa majadiliano ya kimkakati.   | Mikutano ya kawaida huandaliwa, huhudhuriwa na kumbukumbu zake hahihadhiwi vizuri; husababisha maamuzi wazi na ya kimkakati kufanyika na mahusiano yenye tija.   |
| <b>Uhusiano Bainaya Chombo Kikuu cha Utawala na Wafanyakazi</b> | Chombo kikuu cha utawala na wafanyakazi hawaelewani. Mawasilino mabaya na kutokuaminiana vinafafanua uhusiano uliopo.   | Mara nydingi mivutano na kutoelewana kati ya chombo kikuu cha utawala na wafanyakazi hutokea.  | Chombo kikuu cha utawala na wafanyakazi wanawasiliiana vizuri kiasi, lakini kutoelewana hujitokeza mara moja moja.   | Chombo kikuu cha utawala na wafanyakazi wanafanya kazi pamoja vizuri sana kwa lengo la kutimiza dhima ya shirika. Mawasiliano baina yao yako wazi na wafanyakazi na chombo kikubwa cha utawala wanaungwa mkono ipasavyo kufanya kazi zao kwa ufanisi |

## ■ Utawala, unaendelea

|  | Kiwango cha Chini   | Kiwango cha Kawaida   | Kiwango cha Wastani   | Kiwango Kikubwa  |
|--|---|---|---|--|
| <b>Majukumu</b>  | Wajumbe wa chombo<br>kikuu cha utawala<br>hawana uhakika wa<br>wajibu wao na<br>majukumu yao na<br>mchango wao kwa<br>shirika ni mdogo.   | Wajumbe wa chombo<br>kikuu cha utawala<br>sikuzote hawana<br>uhakika wa wajibu wao<br>na wanatoa ushauri na<br>mchango mdogo  | Wajumbe wa chombo<br>kikuu cha utawala<br>wana uhakika wa<br>wajibu wao na mara<br>kwa mara wanatoa<br>ushauri mzuri na<br>unaofaa kwa shirika.   | Wajumbe wa chombo kikuu<br>cha utawala wana uhakika<br>wa wajibu wao na wanatoa<br>mwongozo mzuri kwenye<br>dira na mkakati, na<br>wanatimiza kiutendaji<br>wajibu wao mwininge<br>unaofaa.  |
| <b>Michango<br/>Mbalimbali</b>   | Wajumbe wa chombo<br>kikuu cha utawala<br>hawachangii rasilimali<br>au upatikanaji wa<br>rasilimali.  | Baadhi ya wajumbe wa<br>chombo kikuu cha<br>utawala huchangia<br>rasilimali, na/au<br>upatikanaji wa<br>rasilimali.   | Wajumbe walio<br>wengi wa chombo<br>kikuu cha utawala<br>huchangia rasilimali<br>na/au upatikanaji wa<br>rasilimali.  | Wajumbe wa chombo<br>kikuu cha utawala hutoa<br>michango yenye maana<br>kwenye rasilimali na/au<br>upatikanaji wa rasilimali.  |
| <b>Mkutano<br/>Mkuu wa<br/>Mwaka/<br/>Mkutano<br/>Mkuu wa<br/>Wanachama<br/>Wote (iwapo<br/>upo)</b> | Mkutano Mkuu wa<br>Mwaka hufanyika kwa<br>nadra; mikakati haipitiwi<br>upya; taarifa za kifedha<br>haziwekwi hadharani;<br>wajumbe hawatimizi<br>wajibu wao; mchakato<br>wa kupiga kura<br>hauzingatiwi; miongozo<br>ya uanachama<br>haileweki. | Mkutano Mkuu wa<br>Mwaka hufanyika kila<br>baada ya miaka<br>michache; mkakati<br>unajadiliwa lakini<br>mwafaka huwa<br>haufikiwi; taarifa za<br>kifedha huwa<br>hazivasilishwi<br>kikamilifu; mchakato wa<br>kupiga kura sikuzote<br>huwa hauzingatiwi;<br>miongozo ya<br>uanachama hutoa<br>mwongozo nusu kuhusu<br>wajibu na majukumu. | Mkutano Mkuu wa Mwaka<br>hufanyika mara moja kwa<br>mwaka, japo upangaji<br>ungeweza kuwa imara<br>zaidi; maamuzi ya kimkakati<br>hufanyika lakini majadiliano<br>mara nyangi huwa<br>yanatupwa pembeni; taarifa<br>kamili ya kifedha huwa<br>inawasilishwa lakini<br>ingeweza kupatikana zaidi;<br>mchakato wa kupiga kura<br>huzingatiwa kila mara; mara<br>moja moja huwa<br>kunakuwepo <u>mkanganyiko</u><br>kuhusu wajibu na<br>majukumu ya wajumbe. | Mkutano Mkuu wa Mwaka<br>hufanyika walau mara moja<br>kwa mwaka na unaandaliwa<br>vizuri mapema; wajumbe<br>hudhihirisha uongozi<br>kwenye kufanya maamuzi<br>ya kimkakati; taarifa za<br>kifedha huwasilishwa kwa<br>uwazi na kwa njia ambayo<br>inaziwezesha kupatikana<br>kirahisi; taratiu za kupiga<br>kura na taratibu nyininge<br>hufuatwa kwa kutumia<br>utaratibu maalumu;<br>wajumbe wanafahamu fika<br>wajibu wao na majukumu<br>yao. |

**Maoni:**

## ■ Usimamizi wa Fedha

|  | <b>Kiwango cha Chini</b>   | <b>Kiwango cha Kawaida</b>   | <b>Kiwango cha Wastani</b>   | <b>Kiwango Kikubwa</b>  |
|--|--|--|--|---|
| <b>Mifumo ya Fedha na Udhibiti</b>     | Hakuna mifumo ya kifedha ambayo imehifadhiwa kimaandishi au mifumo ya udhibiti inayoongoza shughuli za kifedha; hakuna taratibu rasmi kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu au kutoa taarifa za kifedha. | Hakuna mifumo ya kifedha ambayo imehifadhiwa kimaandishi au mifumo ya udhibiti inayoongoza shughuli za kifedha; hakuna taratibu rasmi kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu au kutoa taarifa za kifedha. | Mifumo rasmi na udhibiti inaoongoza shughuli za kifedha, kukiwemo na hifadhi ya kumbukumbu na tarataibu wazi. Mifumo inakidhi mahitaji mengi ya wadau mbalimbali lakini bado kuna mapengo.                         | Mifumo imara na mwafaka na udhibiti vipo kuongoza shughuli za kifedha, kukiwemo na taratibu za kina za kuhifadhi kumbukumbu na kudumisha uwazi.   |
| <b>Ujuzi wa Kifedha wa Wafanyakazi</b> | Wafanyakazi hawana maarifa na mafunzo ya kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao  | Wafanyakazi wachache wana maarifa na mafunzo ya kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; pale ambapo kuna sera, hazizingatiwi kwa utaratibu maalumu.                                  | Wafanyakazi wengi wana maarifa na ujuzi muhimu wa kuwawezesha kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; wengi wao wamepata mafunzo kuhusu mifumo ya kifedha ya shirika, wanazingatia sera muda wote. | Wafanyakazi wana maarifa na ujuzi muhimu wa kuwawezesha kusimamia kwa uhodari mkubwa masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; wamepata mafunzo kikamilifu kuhusu mifumo ya kifedha ya shirika na wanazingatia sera kwa kufuata utaratibu maamlumu. |
| <b>Ujuzi wa Kifedha wa Wafanyakazi</b> | Wafanyakazi hawana maarifa na mafunzo ya kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao.   | Wafanyakazi wachache wana maarifa na mafunzo ya kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; pale ambapo kuna sera, hazizingatiwi kwa utaratibu maalumu                                   | Wafanyakazi wengi wana maarifa na ujuzi muhimu wa kuwawezesha kusimamia masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; wengi wao wamepata mafunzo kuhusu mifumo ya kifedha ya shirika, wanazingatia sera muda wote. | Wafanyakazi wana maarifa na ujuzi muhimu wa kuwawezesha kusimamia kwa uhodari mkubwa masuala ya kifedha yanayohusiana na kazi zao; wamepata mafunzo kikamilifu kuhusu mifumo ya kifedha ya shirika na wanazingatia sera kwa kufuata utaratibu maamlumu. |
| <b>Usimamizi wa Bajeti</b>             | Hakuna utayarishaji mipango ya kifedha kishirika au uandaaji bajeti ya shirika; shirika mara nyingi linashindwa kutimiza wajibu wake kifedha.  | Kuna utayarishaji mdogo wa mipango ya kifedha; bajeti hazilinganishwi na matumizi halisi. Shirika kila mara haliwezi kutimiza wajibu wake wote wa kifedha.   | Maandalizi ya bajeti na mipango yanafanyika mara kwa mara, lakini ulinganishaji bajeti-na-matumizi halisi hufanyika kiholela. Shirika mara moja moja hupata hasara kiasi.  | Kuna mipango thabiti ya kifedha na maandalizi ya bajeti, pamoja na ulinganishaji mara kwa mara wa bajeti-na-matumizi halisi. Shirika halipati hasara.   |

## ■ Usimamizi wa Fedha, unaendelea

|  | <b>Kiwango cha Chini</b>  | <b>Kiwango cha Kawaida</b>   | <b>Kiwango cha Wastani</b>  | <b>Kiwango Kikubwa</b>  |
|--|---|--|---|---|
| <b>Ulinganifu kati ya Fedha na Programu Mbalimbali</b> | Bajeti za msingi zinaandalialiwa kwa ajili ya shirika, lakini hazitengenishwi kwa kila programu; utengaji wa bajeti na ufuatiliaji haviviani na vipaumbele nya shirika. | Maandalizi ya bajeti yanagawanywa kiidara na kiprogramu, lakini mfumo wa maandalizi ya bajeti haupatanu utekelezaji wa mradi au masharti ya ufadhilli; utengaji wa bajeti haulingani kikamilifu na vipaumbele nya shirika. | Maandalizi ya bajeti yanapatana na dhima na vipaumbele nya shirika lakini zinabakia hitilafu kwenye jinsi programu mbalimbali zinaweza kufuatilia fedha ambazo zimetengewa, jambo ambalo linasababisha mkanganyiko wakati fulani. | Mifumo ya kifedha na upangaji imetayarishwa kudhihirisha vipaumbele nya shirika. Programu mbalimbali na fedha vinapatana kikamilifu katika ufuatiliaji mapato na matumizi ya fedha. |
| <b>Ukaguzi wa Mahesabu ya Shirika</b>                  | Hakuna taratibu za ukaguzi wa mahesabu kimaandishi na ukaguzi wa mahesabu haufanyiki.   | Ukaguzi wa mahesabu haufanyiki kikamilifu na/ au hufanyika kiholela na masuala yanayoibuliwa sikuzote hayatatuliwi.  | Ukaguzi wa mahesabu huru unafanyika kila mwaka lakini matoeko ya ukaguzi hayatendewi kazi kwa kufuata utaratibu maalumu au kusambazwa mionganoni <u>mwa hadhira</u> husika.   | Ukaguzi wa mahesabu huru unafanyika kila mwaka na matoeko ya ukaguzi yanatendewa kazi na kusambazwa mionganoni mwa hadhira husika.  |

**Maoni:**

## ■ Uchangishaji Fedha na Mahusiano na Mfadhili

|  | <b>Kiwango cha Chini</b>  | <b>Kiwango cha Kawaida</b>   | <b>Kiwango cha Wastani</b>   | <b>Kiwango Kikubwa</b>  |
|--|---|--|--|---|
| <b>Upanuzi wa Upatikanaji Fedha</b>            | Mfadhili mmoja au wawili hutoa msaada kwa kipindi kifupi. Hakuna mkakati wazi wa kuchangisha mapato ya baadaye na hakuna juhud ya kutafuta taasisi mpya na/au wafadhili binafsi.        | Wafadhili wakuu wachache hutoa msaada kwa mradi mwaka baada ya mwaka. Hakuna mpango wa muda mrefu wa kuchangisha fedha na kuna msisitizo mdogo kwenye kubainisha taasisi mpya na/au wafadhili binafsi.                                 | Mkakati wa kuchangisha fedha husababisha kujitekeza taasisi nyngi sana na/au wafadhili binafsi wengi sana ambaeo hutoa misaada yenye masharti nafuu kwa miaka mingi lakini juhud zaidi zinahitajika; vyanzo vipyta vinatafutwa mara moja moja. | Mkakati wa kuchangisha fedha ambao umeandalowi vizuri sana husababisha kupatikana misaada endelevu na tofauti kwa ajili ya kazi za msingi za shirika, zikiwemo taasisi na wafadhili binafsi; vyanzo vipyta vinatafutwa kila mara.                   |
